

---

# Mwanga wa Lugha

---

---

---

---

# Mwanga wa Lugha

**MOI UNIVERSITY**  
**≡ PRESS** 

---

---

Moi University Press, Moi University, Eldoret

© Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,  
Chuo Kikuu cha Moi

Kimechapishwa 2019

Chapa ya Kwanza 2019

ISSN 2412-6993

Kimetoleshwa na:  
Utafiti Foundation  
Outspan, Off Eldoret-Nakuru Road,  
P. O. Box 884 – 30100, Eldoret, Kenya.  
Tel: +254 722 313 515  
Website: [www.utafitifoundation.com](http://www.utafitifoundation.com)

---

---

## Yaliyomo

Utambuzi, Hisia na Mabadiliko ya Kisemantiki katika Leksia za Kiswahili <i>Tirus Mutwiri Gichuru, Kitula King'ei na Ileri Mbaabu</i> .....	1
Literature as Medium for Moral Instruction: A Swahili/Islamic Analysis of Ahmad Nassir's <i>Utenzi wa Mtu ni Utu</i> <i>Amiri Swaleh and Rayya Timammy</i> .....	17
Changamoto Zinzokumba Uchanganuzi, Ufasiri na Ufunzaji Ushairi wa Kiswahili katika Shule za Upili Nchini Kenya <i>Gakuo J. Kariuki</i> .....	31
Software Localization: An Exploration of the Problems Encountered by Localizers in Transferring Messages from English into Kiswahili <i>Rufus Karani Munyua, P. I. Iribemwangi and Tom M. Olali</i> .....	45
Feminism Ideology and Institution of Patriarchy in African Novel: Analysis of Selected Works of Women Writers and Gynandrists <i>Albert Rutere</i> .....	61
Athari ya Ukiushi wa Kisarufi katika Tafsiri ya Matini katika Majukwaa ya Kidijiti <i>Mark A. Odawo, Carren Nyandiba na James Omari Ontieri</i> .....	71
Juhudi za Kukabiliana na Kuangamia kwa Lugha za Kiafrika <i>S. M. Obuchi</i> .....	91
Metaphorical Construction and Interpretation of Kiswahili Compound and Complex Clauses <i>Mary Njeri Ndung'u and John H. Habwe</i> .....	105
Tathmini ya Mikakati ya Tafsiri ya <i>Vinay na Derbelnet</i> (2004) katika Tafsiri ya <i>A Good Day</i> (2019) <i>Sarah Ndanu M. Ngesu, Pendo Salu Malangwa na Mosol Kandagor</i> .....	129
Mtagusano wa Uforensiki na Riwaya ya Kiswahili: Mfano kutoka Riwaya ya 'Mzimu wa Watu wa Kale' <i>Neema Julius Luhwago</i> .....	153

---

Tahakiki Linganishi ya Motifu Zinazobainika katika Tendi za <i>Mikidadi na Mayasa na Kalevala</i> <i>Jackson Ndung'u Mwangi, Wendo Nabea na Sheila P. Wandera-Simwa</i> .....	169
Muakiso wa Uhalisi wa Kauli za Mhusika Mlevi na Uchagizaji wa Tafsiri kwa Msomaji katika Fasihi ya Kiswahili <i>Gerephace Mwangosi na Lazaro Mlelwa</i> .....	181
Vipashio vya Lugha Vinavyosawiri Ubabedume katika Majigambo ya <i>Miviga ya Shilembe</i> na <i>Mchezasili wa Mayo</i> Miongoni mwa Waisukha Nchini Kenya <i>Mary Lukamika Kibigo, Susan C. Choge na Fred Wanjala Simiyu</i> .....	201
Itikadi katika Riwaya za <i>Dunia Yao</i> (2006) na <i>Mhanga Nafsi Yangu</i> (2013) za S. A. Mohamed <i>Murithi Joseph Jesse na Kitula King'ei</i> .....	211
Uundaji wa Lakabu za EkeGusii <i>Milcah Nyathira</i> .....	225
Masculine and Feminine Constructions of Migration in Swahili Literature: <i>Mbali na Nyumbani</i> and <i>Mhanga Nafsi Yangu</i> <i>Zaja Omboga</i> .....	235
Nafasi ya Kiswahili katika Mandhari-Lugha: Uchambuzi Kifani wa Mabango ya Matangazo ya Makampuni ya Mawasilino ya Simu <i>Gervas A. Kawonga</i> .....	259
Mchango wa Kazi Teule za Fasihi katika Kukabiliana na Janga la UKIMWI <i>Charles Kituni Wasike, Mosol Kandagor na S. M. Obuchi</i> .....	275

---

### **Kamati ya Uhariri**

Prof. Nathan Ogechi (Mhariri Mkuu)	Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi
Dkt. Mosol Kandagor (Mhariri Msaidizi)	Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi
Dkt. Makoti Vifu	Chuo Kikuu cha Machakos
Dkt. S. M. Obuchi	Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi
Dkt. Allan Opijah	Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi
Dkt. Magdalene Wafula	Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi
Dkt. Mary Lonyangapuo	Idara ya Isimu na Lugha Nyingine za Kigeni, Chuo Kikuu cha Moi
Dkt. James O. Ontieri	Chuo Kikuu cha Maasai Mara
Dkt. Emmanuel Satia	Idara ya Isimu na Lugha Nyingine za Kigeni, Chuo Kikuu cha Moi
Dkt. Bernard Toboso	Chuo Kikuu Kishirikishi cha Alupe
Dkt. Leonard Chacha Mwita	Chuo Kikuu cha Kenyatta

### **Washauri wa Wahariri**

Prof. M. H. Abdulaziz	Chuo Kikuu cha Nairobi
Prof. John Habwe	Chuo Kikuu cha Nairobi
Prof. Inyani Simala	Kamisheni ya Kiswahili-Afrika (KAKAMA), Zanzibar
Prof. E. S. Mohochi	Chuo Kikuu cha Rongo
Prof. Florence Indede	Chuo Kikuu cha Maseno
Prof. P. I. Iribemwangi	Chuo Kikuu cha Nairobi
Prof. Aldin Mutembei	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania
Prof. Peter Simatei	Chuo Kikuu cha Moi
Prof. Mellitus Wanyama	Chuo Kikuu cha Kabarak
Prof. Clarissa Vierke	Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani
Dkt. Pendo S. Malangwa	Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam, Tanzania
Dkt. Ayub Mukhwana	Chuo Kikuu cha Nairobi

---

## Kuhusu Jarida

**Mwanga wa Lugha** ni jarida la Idara ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika katika Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret-Kenya. Jarida hili huchapisha makala za lugha, isimu na fasihi. Aidha, jarida hili huchapishwa mara mbili kwa mwaka, yaani Aprili na Septemba.

### Maelekezo kwa Waandishi wa Makala

Waandishi wanaombwa kuwasilisha makala zao kwa kuzingatia maagizo yafuatayo:

1. Makala yawe na kichwa, jina la mwandishi, chuo, taasisi au shirika analofanyia kazi, anwani ya posta na barua pepe, nambari ya simu na taarifa fupi kuhusu mwandishi. Taarifa hizi zitokee kwenye ukurasa wa kwanza.
2. Makala yapigwe chapa kwa kutumia programu ya MS WORD, kwa kuzingatia utaratibu wa Times New Roman kwenye umbo la A4, kukiwa na nafasi ya 1.5 baina ya mistari na maandishi yawe ni ya kiwango cha 12.
3. Ikisiri iandikwe kwa kutumia italiki, isizidi maneno 200 na itokee mwanzoni mwa makala, chini ya taarifa zilizotajwa hapo juu (1).
4. Idadi ya maneno isizidi 6000.
5. Lugha ya jarida iwe ni Kiswahili tu. Hata hivyo makala yaliyoandikwa kwa Kiingereza yanaweza kufikiriwa.
6. Marejeleo yaandikwe kwa kutumia mfumo wa APA.
7. Ikiwa ni lazima mwandishi atumie tanbihi, tunapendekeza matumizi ya tanbihi mwisho badala ya tanbihi chini.

### Wasiliana Nasi Kupitia:

Ama  
Mhariri Mkuu  
Jarida la Mwanga wa Lugha  
Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika  
Chuo Kikuu cha Moi  
S.L.P 3900-30100  
Eldoret-Kenya.

### Au

[Jaridalamwangawalugha@gmail.com](mailto:Jaridalamwangawalugha@gmail.com) na [jaridalamwangawalugha@mu.ac.ke](mailto:jaridalamwangawalugha@mu.ac.ke)

---



---

## Tahariri

Toleo hili linajumuisha jumla ya makala ambayo yanatanda katika taaluma mbalimbali za lugha na fasihi. Makala ya Tirus Mutwiri Gichuru, Kitula King'ei na Ireri Mbaabu yamebainisha kuwa maarifa na tajriba zilizofichamwa kwenye utambuzi huwa nguzo muhimu katika kuleta mabadiliko ya maana za leksia. Imebainika wazi kuwa muundo wa maana na maumbile ya mwanadamu hasa hisia zake tano na ufasili wake wa ulimwengu husaidia mwanadamu kukabiliana na dhana mpya zinazoibuka katika mazingira halisi na ya kidhahania. Nao Amiri Swaleh and Rayya Timammy wamechambua *utendi wa Mtu ni Utu* (1978) uliotungwa na Ahmad Nassir Juma Bhalo. Waandishi wameangazia mafunzo makuu yanayojitokeza katika utendi huu; mafunzo ambayo yanakuza maadili ya kijamii. Uchambuzi huu umeegemea misingi ya Dini ya Kiislamu, kulingana na tajriba na maarifa ya mtunzi wa utendi huu.

Makala ya Gakuo J. Kariuki yanaangazia baadhi ya changamoto zinazokumba taaluma ya ufasiri, uelewekaji na ufundishaji wa somo la ushairi katika shule za sekondari nchini Kenya. Mawazo na kauli zinazoshereheshewa katika makala haya zinazotokana na utafiti wa kisayansi uliofanywa katika kaunti mbili za Mombasa na Trans Nzoia. Rufus Karani Munyua, P. I. Iribemwangi na Tom M. Olali wameshughulikia suala la utafsiri kwa kudai kwamba chochote kinachoweza kusemwa katika lugha moja kinaweza pia kusemwa katika lugha nyingine. Waandishi hawa wamewarejelea wataalamu waliotukuka katika taaluma ya tafsiri kama vile Catford, Nida na Newmark kuhusiana na masuala wanayoyaibua.

Naye Albert Rutere ameshughulikia matumizi ya nadharia ya ufeministi katika usomaji na uhakiki wa riwaya ya kiafrika kwa kurejelea kazi teule za waandishi wa kike wa kiafrika kwa kujikita kwenye mirengo ya Anglofoni na vilevile ya Frankofoni barani Afrika. Mwandishi amerejelea Riwaya za Ngugi Wa Thiongo (*Devil on the Cross*), Buchi Emecheta (*The Joys of Motherhood*), Tsitsi Dangarembga (*Nervous Conditions*), Sembene Ousmane (*God's Bits of Wood*), Mongo Beti (*Perpetua*) na Mariama Ba (*So Long a Letter*). Mark A. Odawo, Carren Nyandiba na James Omari Ontieri wameangazia jinsi ukiushi wa kisarufi katika tafsiri huathiri maana ya ML. Ukiushi uliotatiza maana ya matini zilizotafsiriwa katika ML ulitokana na tofauti za kiisimu kati ya LC na LL zilizopelekea miundo na ruwaza za kisintaksia za LC kulazimishwa katika LL; makosa ya kiupatanishi, kiuakifishaji, kiunyambulishi na ya kitahajia.

S. M. Obuchi anajadili matokeo mawili ya mtagusano lugha: kuhatarishwa kwa lugha na kufa kwa lugha. Katika uhatarishwaji wa lugha, kimsingi, mwandishi amejadili dhana mbalimbali kama vile sababu za uhatarishwaji lugha, athari za uhatarishwaji lugha, vigezo vya kutambua ikiwa lugha imehatarishwa, mchango wa UNESCO katika kuokoa lugha zilizo hatarini na mifano ya lugha zilizo hatarini katika bara la Afrika. Mary Njeri Ndung'u na John H. Habwe wameshughulikia miundo ya kimafumbo ya Kiswahili katika kiwango cha Kirai. Waandishi hawa walilenga katika kuonyesha namna ambavyo Kiswahili hudhihirisha semi za kimafumbo katika ngazi ya

---

Kirai na jinsi maana hujidhihirisha katika kiwango hicho. Makala ya Sarah Ndanu M. Ngesu, Pendo Salu Malangwa na Mosol Kandagor yamebaini kwamba uteuzi wa mikakati ya tafsiri ina athari chanya na hasi katika uhawilishaji wa ujumbe. Mikakati iliyotumiwa ilifanikiwa kuhawilisha ujumbe wa mwandishi kwenda lugha lengwa kwa njia inayofaa, lakini pia ilikuwa na athari hasi kwa kupotosha ujumbe kama ilivyoelezwa hapo awali hususan matumizi ya mkakati wa tafsiri sisisi katika tafsiri ya vipengele vya kiutamaduni.

Makala ya Neema Julius Luhwago yameonesha mtagusano wa uforensiki kama unavyodhihirika katika riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale ambapo unathibitisha uwepo wa mwingiliano wa taaluma hizi mbili yaani fasihi na uforensiki kujitokeza katika riwaya. Mwandishi ameonyesha kuwa fasihi, kama kilelezo cha kisanaa kitumiacho lugha kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa, hutegemea ujenzi wa kazi yake kupitia matukio, wahusika, muktadha wa jamii unaojegwa na wahusika na mahusiano yao katika jamii. Makala ya Jackson Ndung’u Mwangi, Wendo Nabea na Sheila P. Wandera-Simwa yanabainisha wazi kuwa kuna uwezekano wa kazi mbili za fasihi kutoka maeneo tofauti ya kijiografia kuathiriana na kuingiliana kwa kiwango fulani. Makala haya yamebaini kuwa kuna motifu nyingi mno zinazolingiliana baina ya tendi za Kimagharibi na zile za Kiafrika. Waandishi wamejikita katika Utendi wa Kalevala na Utendi wa Mikidadi na Mayasa.

Nao Gerephace Mwangosi na Lazaro Mlelwa wamejadili muakiso wa ukweli wa kauli za mlevi na namna zinavyochagiza tafsiri kwa msomaji au msikilizaji kwa kurejelea vitabu teule. Makala haya yamezingatia uhalisi wa kauli za mhusika mlevi kwa kurejelea tamthilia teule. Pia, yametalii jinsi matendo na kauli za mhusika mlevi zinavyochagiza tafsiri mbalimbali kwa wasomaji na wasikilizaji. Mary Lukamika Kibigo, Susan C. Choge na Fred Wanjala Simiyu wamedhihirisha kuwa miviga ya *Shilembe* na mchezasili wa *Mayo* si sherehe tu bali ni majukwaa ambayo Waisukha hutumia ili kudhihirisha ubabedume wao kupitia vipashio teule vya lugha katika majigambo yanayoghanwa katika sherehe hizi. Kwa kutumia vipashio kadhaa vya lugha kisanii katika majigambo, Waisukha wamedhihirisha kwamba ubabedume ni sifa ambayo bado inaamua mahusiano ya kijinsia katika jamii. Kando na majigambo kuwa jukwaa la kujadilia masuala ya kijinsia, yanatumika pia kujadilia masuala ya ukoo, uzazi na mapenzi.

Murithi Joseph Jesse na Kitula King’ei wameonesha jinsi itikadi ya utandawazi inajitokeza katika riwaya ya *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* kama inavyodhihirishwa katika vipengele vya mfumo wa kiuchumi, kielimu, kindoa, kidini, asasi za utawala, kimaadili na mfumo wa kuumeni. Makala yamependekeza mapinduzi kufanyika ili kusuluhisha matatizo yao kwani kutorokea mataifa ya Ulaya hakubadilishi hali. Naye Milcah Nyathira amedhihirisha kuwa wachezaji kandanda wa jamii ya Abagusii wana lakabu ambazo wao hutumia sambamba na majina yao halisia. Lakabu hizi zina maumbo mahususi. Makala haya pia yameangazia mbinu kadha wa kadha zinazotumika katika uundaji wa lakabu mbalimbali. Zaja Omboga ameangazia riwaya mbili ambazo zinaelekea kulandana kuhusiana na yaliyomo katika masimulizi

---

ya *Mbali na Nyumbani* na vilevile *Mhanga nafsi yangu*. Kazi hizi mbili zinakuza maudhui yaleyale kuhusu siasa, uchumi, ajira, miongoni mwa masuala mengine.

Gervas A. Kawonga amechunguza nafasi ya Kiswahili kimatumizi katika mandhari-lugha ya Jiji la Mbeya nchini Tanzania. Uchambuzi wa mabango ya makampuni ya mawasiliano ya simu umefanyika kwa kutumia zanatepe ya Programu Tarakilishi ya Takwimu (PTT). Vipengele vilivyochunguzwa ni mpangilio wa lugha, ukubwa wa maandishi na idadi ya maneno. Matokeo haya yanatofautiana na tafiti nyingi tangulizi kuhusu nafasi ya Kiswahili katika mandhari-lugha nchini Tanzania. Nao Charles Kituni Wasike, Mosol Kandagor na S. M. Obuchi wamejadili kwa kina namna ambavyo maandishi teule ya fasihi andishi yametumika kwenye vita vya kukabiliana na ugonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya njia zilizopendekezwa kupambana na UKIMWI ni pamoja na kuepuka uasherati, kupinga unyanyapaa, kuzingatia maadili bora katika jamii, kuwa waaminifu katika maisha ya ndoa miongoni mwa zingine.

---

## **Kuwahusu Waandishi wa Makala**

**Albert Rutere**

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Laikipia

**Amiri Swaleh**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Nairobi

**Carren Nyandiba**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Rongo

**Charles Kituni Wasike**

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Moi

**Fred Wanjala Simiyu**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Kibabii

**Gakuo J. Kariuki**

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Gerephace Mwangosi**

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha, Iringa

**Gervas A. Kawonga**

Mhadhiri na Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Ileri Mbaabu**

Profesa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Jackson Ndung'u Mwangi**

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Laikipia

**James Omari Ontieri**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara

**John H. Habwe**

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Nairobi

---

**Kitula King’ei**

Profesa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Lazaro Mlelwa**

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Kikatoliki Ruaha, Iringa

**Mark A. Odawo**

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Rongo

**Mary Lukamika Kibigo**

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Sayanzi na Teknolojia cha Masinde Muliro

**Mary Njeri Ndung’u**

Mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi

**Milcah Nyathira**

Mzamili katika Chuo Kikuu Cha Kisii

**Mosol Kandagor**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Moi

**Murithi Joseph Jesse**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Neema Julius Luhwago**

Mhadhiri na Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Dodoma

**P. I. Iribemwangi**

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Nairobi

**Pendo Salu Malangwa**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Rayya Timammy**

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Nairobi

---

**Rufus Karani Munyua**

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Nairobi

**S. M. Obuchi**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Moi

**Sarah Ndanu M. Ngesu**

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Sheila P. Wandera-Simwa**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Laikipia

**Susan C. Choge**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Sayanzi na Teknolojia cha Masinde Muliro

**Tirus Mutwiri Gichuru**

Mzamifu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta

**Tom M. Olali**

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Nairobi

**Wendo Nabea**

Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Laikipia

**Zaja Omboga**

Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Nairobi